

USA WIRI WA WAHUSIKA KATIKA HADITHI FUPI YA KISWAHILI

E.S. Mohochi

Idara ya Lughya na Isimu, Chuo Kikuu cha Egerton

Ikisiri

Hadithi fupi ni kazi ya fasihi ambayo imefaulu kusimama kidete kama utanze mahsusili licha ya msimamo wa awali wa wataalamu wengi walioiona kama sehemu tu ya riwaya. Kwa hakika wapo baadhi ambao waliiona hadithi fupi kama riwaya pungufu. Mojawapo kati ya kipengele muhimu kinachodhahirisha huo upkee wa hadithi fupi ni uchoraji na usawiri wake wa wahusika. Makala hii imelengwa kujadili usawiri wa wahusika katika hadithi fupi. Hili litatekelezwa kwa kuchunguza maendeleo ya hadithi fupi katika kipengele hicho kimuhtasari kabla ya kujadili kwa undani sifa mbalimbali za wahusika wa hadithi fupi ya Kiswahili na hatimaye kuonyesha jinsi, kupitia kwa usawiri wake tofauti wa wahusika, hadithi fupi inafaulu kuwasilisha ujumbe muhimu kuhusu jamii kama tanzu nyingine za fasihi.

UTANGULIZI

Mwandishi wa kazi ya fasihi hutumia wahusika, anaowaumba yeye, kuyaeleza matukio anayotaka kuyawasilisha kwa hadhira yake. Kwa hakika wahusika ni viumbe wa akilini mwa msanii, ambao huwekwa katika maandishi ili kutekeleza wajibu maalum wa kuwa wakala wa mwandishi. Anawatumia kuyakuza na kuyasafirisha maudhui yake hadi kwa wasomaji wake. Hulka, sura, mawazo, matendo pamoja na kauli za wahusika, kwa kawaida, huchotwa kutokana na maisha ya jamii huku mwandishi akiongozwa na lengo kuu la kazi yake.

Kazi mbalimbali za fasihi zina kaida kadha wa kadha ambazo zinaongoza watanzi wa kazi hizo. Japo kimsingi malighafi wanayoitumia watanzi wote wa kazi tofauti za fasihi ni ile ile, hizo kaida ndizo huongoza namna ambavyo watanzi hao watachota kutoka kwa malighafi hiyo na aina ya umbo la kazi ya fasihi ambalo wataibuka nalo. Katika wahusika, kama ilivyo katika vipengele vingine vijengavyo kazi ya fasihi, kaida hizo huathiri sana ujenzi wa wahusika. Kwa maana hiyo, hadithi fupi inazo kaida maalum zinazoongoza ujenzi na uwasilishaji wa wahusika wake, jambo ambalo huchangia kuifanya tofauti na kazi nyingine za fasihi. Kabla ya kuzitizama kaida hizo na kuona jinsi zinavyoongoza ujenzi wa hadithi fupi mahsusili, tutaangaza dhana ya wahusika kwa ujumla katika fasihi.

Dhana na Dhima ya Wahusika

Mwandishi ashikapo kalamu na karatasi, au kifaa kingine chochote kuandika hadithi fupi au kazi nyingine ya fasihi, ana jambo maalum ambalo limemkereketa kiasi cha kumfanya atake kuliwasilisha kwa jamii. Tofauti na waandishi wengine, mfano wale wa habari au hotuba ya kawaida, mwandishi wa fasihi hutumia wahusika kama maajenti wake kwani hajielezi moja kwa moja.

Dhana ya Wahusika

Kuna kongamano mionganoni mwa wataalamu wa fasihi kwamba wahusika ni viumbe wa mwandishi watumiwao kuyaeleza na kuyasema aliyokusudia. Senkoro (1982:8) anatoa maelezo yafuatayo:

Wahusika ni watu, ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu, katika kazi za fasihi.

Fasihi hutegemea uwezo wa msanii wa kuzua au kubuni kutokana na yale yanayojitokeza katika jamii. Anapobuni kutokana na matukio katika jamii, analazimika kuwaumba wahusika na kuwatumia kuyaeleza matukio hayo. Vile vile, wahusika huwa matokeo ya akili ya mwandishi kwani ni viumbe wa akilini mwa msanii, ambao huwekwa katika maandishi ili kutekeleza wajibu maalum. Kwa hakika, hata mwandishi anapoandika kuhusu tukio la kihistoria na hivyo akawa na mhusika wa kihistoria, bado anatumia usanii wake kumuumba upya huyo mhusika wa kihistoria.

Katika uumbaji wa hao wahusika, mwandishi huchota hulka; sura, mawazo, matendo pamoja na kauli zao kutokana na maisha ya jamii yake akiongozwa na lengo lake. Katika misingi hiyo, wahusika si tofauti sana na dhamira kuu ya msanii ambayo pia, mara kwa mara, huchotwa kutoka kwa maisha ya jamii. Wahusika huweza kuwa watu, wanyama, miti, mashetani, miungu, wadudu na viumbe wengine. Kwa mfano, ngano zilitumia viumbe mbalimbali kama vile mimea, miungu, mazimwi na wanyama kama wahusika wakuu. Viumbe hawa walitumiwa kuwakilisha matendo na mienendo ya binadamu. Kutokana na mabadiliko katika fasihi, waandishi wengi hivi sasa hutuchorea zaidi wahusika watu katika misingi ya kihalisia. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya hadithi fupi na kazi nyingine ambazo zimetumia wahusika wanyama.

Dhima ya Wahusika

Ujumbe wa mwandishi hutufikia wasomaji au wapokeaji kupitia kwa munungumzo na matendo ya wahusikka wake. Fauka ya hayo, wahusika humuika kuwakilisha dhana, watu na sifa mbalimbali katika jamii (Msokile, 1992). Kwa jumla, wahusika hutumiwa kuarifu, kufurahisha, kufundisha, na

kufahamisha iwa hadithi hutu
Kimsingi mbalimbali wa hiyo. Upo wa uwakilishaji mbalimbali. Kmwingine wa kama wanaja mbalimbali ya wahusika katika kuwafanya wa

Wahusika tunavyowaele mwandishi ar mhusika wakuchangamano akatufahamish twaweza kulinwengu wa

Wasanii Wanatuwezes hulka na mat hisia mbalimbali fasihi. Kutok tukachecha na masikitiko ya

Uumbaji wa Kuhusu uumb zao mbalimb ni uteuzi wa yake katika na amebanwa na jamii humtai Kutokana na Ili kulifikia vipengele ka ndizo mbinu

kufahamisha msomaji jambo au kufafanua imani fulani. Kwa kawaida, mhusika wa hadithi hutekeleza majukumu kadhaa katika uhusika wake.

Kimsingi, kazi za fasihi ni mkusanyiko wa matendo tofauti ya wahusika mbalimbali walio na nafasi maalum katika kuendeleza ploti ya matini ya kazi hiyo. Upo wakati ambapo wahusika hutumiwa kuwakilisha fikra za mwandishi, uwakilishaji ambao hutokana na jinsi ambavyo msanii amewateulia sifa mbalimbali. Kwa kawaida, waandishi huumba watu wanaowafahamu na wakati mwingine wakajiumba wenyewe katika maandishi yao. Baadhi ya waandishi, kama wanajamii wengine, wana misimamo inayojulikana kuhusu maswala mbalimbali yaihusuyo jamii. Hutokea wakati ambapo waandishi hao huwatumia wahusika katika kazi zao kuieleza na kuitetea hiyo misimamo yao na, hivyo, kuwfanya wahusika hao kutekeleza wajibu wa kuwa wasemaji wa mwandishi.

Wahusika wa kazi za fasihi hutuwezesha kuwaelewa binadamu kuliko tunavyowaelewa watu tunaohusiana nao kila siku. Sababu ya hali hii ni kuwa mwandishi ana uwezo wa kutuonyesha maisha ya siri na mawazo ya ndani ya mhusika wake. Perrine (1960) anasema kuwa wahusika hutuwezesha kujua uchangamano wa mahusiano ya binadamu vizuri zaidi kwani msanii anaweza akatufahamisha mawazo ya mhusika wake. Ilivyo katika maisha ya kawaida, twaweza kukisia tu anachokiwaza mwezetu. Kwa maoni yake, watu na ulimwengu wao hueleweka bora zaidi katika kazi za fasihi.

Wasanii hutumia wahusika wao kutekeleza majukumu mbalimbali. Wanatuwezesha kuupata ujumbe uliopo katika kazi zao pamoja na kutufunulia hulka na matendo ya binadamu wazi zaidi. Aidha, wahusika hutumiwa kuibua hisia mbalimbali kwa wasomaji, hisia ambazo huyafanikisha maudhui ya kazi ya fasihi. Kutokana na hali hii, tunaweza kujitambulisha na wahusika maalum; tukachecha nao, tukahuzunika nao, au kuungana nao katika matarajio na masikitiko yao.

Uumbaji wa Wahusika

Kuhusu uumbaji, msanii hukabiliwa na maswali mawili muhimu. Kwanza ni sifa zao mbalimbali; urefu, rangi ya ngozi, matendo na mienendo yao kijumla. Pili, ni uteuzi wa mbinu atakayoitumia kuwapa uhai na kuwawasilisha kwa hadhira yake katika maandishi. Ingawa wahusika ni viumbe wa mwandishi, msanii huwa amebanwa na jamii katika uumbaji wa wahusika wake, kwani sehemu kubwa ya jamii humtarajia kuibua wahusika watakaolingana na hali halisi maishani. Kutokana na hilo, uteuzi wa sifa mbalimbali za wahusika huhitaji makini sana. Ili kulifikia lengo hilo, waandishi wa kazi mbalimbali za fasihi wanatumia vipengele kadha wa kadha kuwajenga na kuwapa uhai wahusika wao. Zifuatazo ndizo mbinu za msingi;

Lugha na Fikra

Mwandishi huwapa wahusika wake fikra na lugha huku akiongozwa na ujunbe na, muhimu zaidi, hadhira anayoikusudia ujumbe wake. Lugha na fikra za mhusika zaweza kujitokeza kutoka kinywani mwa mhusika mwenyewe, ama kupitia kwa msanii. Lugha anayoitumia mhusika ni kipengele muhimu kiwezacho kutufunulia mengi kumhusu mhusika pamoja na uhusiano wake na wenzake.

Kwa hali hiyo, inamuwia muhimu msanii kuoanisha matumizi ya lugha ya wahusika wake na miktadha mbalimbali katika kazi yake. Kwa mfano, katika *Gamba la Nyoka*, tunakuta matumizi tofauti ya lugha baina ya wazee na vijana. Wazee wamepewa lugha nzito yenye methali na nahau nyingi ilhali Mamboleo na Mambosasa, amba ni vijana wasomi, wanatumia lugha kwa kuchanganya ndimi. Ni jambo la kawaida maishani kwa vijana kuchanganya ndimi katika mazungumzo yao kama mfano mwininge wa Sosy na Ray katika *Tazama Mbele* (1980) unavyodhihirisha.

Wasifu (Umbo)

Neno wasifu linatumika hapa kwa maana ya ufanuzi wa nje wa mhusika. Ya muhimu ni yale yawezayo kuonekana wazi wazi; kama umbo la mwili wake. Je, mhusika ni mrefu, mnene, mweupe, mweusi au vipi? Anavaa mavazi ya aina gani? Maeleo hayo yote hutusaidia sana kuwaelewa wahusika wa fasihi, hali ambayo huwezeshwa na tajriba yetu maishani. Kwa mfano, tunapoelezwa aina ya nyumba anamoishi mhusika fulani, tunaihusisha na hali halisi maishani na kumweka katika tabaka lake. Mathalan, katika hadithi ya "Mke Wangu", mhusika wa M.S. Abdulla anaeleza kuwa, baada ya kuoa, wazazi wake walimtengenye na mkewe vyumba vitatu ghorofani. Walipikiwa chakula, na nguo zao zilioshwa na mtumishi. Maeleo haya yanatuchorea picha maalum ya maisha ya kitajiri waliyoishi hao maharusi.

Matendo

Tunaposoma kuhusu matendo ya wahusika tunaathirika sana na, wakati mwininge, kuhisi kama kwamba tunayashuhudia matendo hayo. Athari hiyo hutuongoza kumwelewa zaidi mhusika huyo. Kwa mfano, katika tamthilia ya *Kinjeketile*, Hussein amechora Kinjeketile kwa kutumia matendo mbalimbali ambayo yanakuza na kuuimarisha uwezo wake. Anaingia mtoni na kuibuka huada ya siku kadhaa akiwa mkavu kabisa na nyumba yake inafuka moshi. Matendo kama hayo hutufanya tumuelewe kama mhusika mwenye uwezo na nguo maalum kwani kila tunapoyafikiria yote hayo, yanaonekana kama mambo yasiyo ya kawaida maishani.

Uteuzi wa Majina

Jina ni kipengele muhimu anachokitumia mwanafasihi katika herkisi za kumuumba na kumfanua mhusika vilivyo. Hili humaanisha kuwa kuna umuhimu wa kufanya uteuzi mwafaka wa majina ya watusika. Baadhi ya watusika hupewa majina ya kimajazi ambayo hutuashiria tabia na mienendo yao na hivyo kusaidia kueleza ujumbe wa mwandishi. Aidha, majina kama hayo huamsha shauku yetu ya kutaka kujuu hasa mienendo yanayoiwakilisha. Shaaban ni mwandishi ambaye ametumia sana aina hii ya majina katika kazi zake. Kuna majivuno katika *Kusadikika* (1970), na wengine kama; Utubora, Adili, na Karama. Naye Mkangi (1985) ametumia mchanganyiko wa majazi na jazanda anapowaita watusika wake Matope na Jasho katika riwaya ya *Mafuta*.

Kwa kiasi kikubwa, waandishi wengi wametumia majina ya kawaida kuwarejelea watusika wao. Haya ni majina ambayo tunakumbana nayo kila siku maishani na, wakati mwingine, hali hii hutufanya tujihusishe zaidi na watusika hao na kuwaona kama watu wa kawaida katika mazingira yanayotuzunguka. Mifano yao katika fasihi ya Kiswahili ni mingi sana: kuna Rehema, Rosa, Nyambura, Zuberi, Zakaria na kadhalika. Katika kundi hili, kuna pia watusika wanaotumia majina ya watu walioishi katika kipindi maalum cha wakati, kama vile Kinjeketile wa *Kinjeketile* (1969) na Kimathi katika *Mzalendo Kimathi* (1976). Hata hivyo watusika hao si sawa na watu walioishi kikweli kama shilingi kwa ya pili bali ni watu wa kisanii. Katika kipengele hiki cha uteuzi wa majina, kuna pia watusika wanaotumia majina ya wanyama. Hali hii ilijitokeza zaidi katika fasihi simulizi ambapo wanyama na viumbe wengine walitumiwa kama watusika kwa kuchorwa kudhihirisha tabia na mienendo ya binadamu. Hata katika fasihi andishi, majina kama haya yametumika ili kuwawezesha waandishi kuihakiki na kuikisoa jamii bila kujiingiza matatani. Kwa mfano, *Shamba la Wanyama* (1967) pamoja na "Dua la Kuku Lilivyompata Mwewe".

Uwasilishaji wa Watusika

Baada ya kuwaumba watusika wake (au labda baada ya kufikiria aina ya watusika atakaowatumia) kulingana na mahitaji ya maudhui ya kazi anayoiandika, mwandishi hubakia na jukumu la kuwasilisha watusika wake kwa namna ambayo watazua athari aliyoinsua kwa wasomaji wake. Mbinu mbalimbali za uwasilishaji hutumika, na kwa vile zinatofautiana, msanii wa fasihi anapaswa kuteua ile itakayomfaa zaidi

Uwasilishaji Dhahiri

Huu ni uwasilishaji wa kimaelezo ambapo mwandishi hutuleza kumhusu mhusika wake. Kutokana na hayo maelezo ya msanii, inakuwa rahisi kwetu

wasomaji kumjua mhusika huyo barabara hata kabla ya kukutana naye hadithini. Hali hii inatokana na ule uhuru wa mwandishi kumwingia mhusika akilini na kutufunulia kila kitu, hata mawazo yake. Aidha, mwandishi anaweza kumweleza mhusika wake kwa mapana na mrefu kiumbo kwa sababu anawasilishwa kwa maelezo ya moja kwa moja. Iwapo mhusika ameelezwa kikamilifu mwanzoni mwa hadithi, tunamfahamu kiasi kwamba, kadri ya hadithi inavyoendelea hatuhitaji mengi ya ziada kumhusu. Msokile (1992) anasema kuwa, kwa kuelezw sifa na matendo wazi wazi, wasomaji hupunguziwa taabu kwani wanawaelewa wahusika kwa urahisi. Hata hivyo, hali hiyo huipunguzia fasihi uzuri wake wa kisanaa kwa sababu msomaji anapaswa kutafakari na kuunga vidokezo vya hapa na pale ili kuweza kumjua mhusika viliyvo. Kila kitu kikielezw tutabaki kuisoma ripoti ya mwandishi badala ya fasihi.

Ingawaje mbinu hii humsaidia msanii kulifika lengo lake, inapaswa kutumiwa kwa uangalifu mkubwa sana kwa sababu inaweza ikatinga ufanisi wa mwandishi. Scott na Madden (1960:63) wanatoa maoni yafuatayo kuhusu hali hiyo:

Ni muhimu tukumbuke kuwa ni bora mwandishi asitueleze bali atuonyeshe. Badala ya kutwambia wakati wa kufurahi au kuhuzunika, atuchoree hali ambayo itaibua hisia mbalimbali kwetu. Wasomaji wapaswa kutafakari ili kuielewa kaziya msanii.

La muhimu ni ile hali ya msomaji kuachiwa nafasi ya kuyafumbua mafumbo ya mwandishi. Kwa hivyo ufahamu wetu wa wahusika utakuwa bora zaidi na wenye kuburudisha iwapo utatokana na uchunguzi wetu wenyewe bila kutegemea maelezo ya mwandishi. Pamoja na ukweli huo, maelezo ya mwandishi hutekeleza jukumu muhimu. Cha msingi ni kuwa yapaswa kupunguzwa lakini yasipunguzwe kiasi cha kuleta utata katika uelewekaji wa kazi hiyo kwa ujumla. Mfano wa mhusika aliyewasilishwa kwa maelezo dhahiri ni Siti katika *Wasifu wa Siti Binti Saad* (1952). Katika riwaya hii, Shaaban amejitwika jukumu la kumweleza na kumpambanua mhusika wake kwa mapana na mrefu. Ufahamu wetu wa Siti umetokana na mwandishi isipokuwa kidogo tu anapojifafanua mwenyewe katika nyimbo za kuwajibu mahasidi wake.

Wahusika Kujifafanua

Wahusika wa kazi mbalimbali za fasihi wanaweza kujifafanua wenyewe kwa wasomaji wa kazi hizo kwa njia mbili kuu. Mhusika anaweza kujifafanua wenyewe ama akafafanuliwa na wahusika wenzake.

Mhusika Kujifafanua Mwenyewe

Mbinu hii imeitwa uwasilishaji wa kidrama kwa sababu mwandishi humpatia mhusika au watusika nafasi ya kujidhihirisha badala ya kuwaeleza. Katika matumizi ya mbinu hii, mwandishi hutuonyesha badala ya kutuambia, na hivyo msomaji anapata fursa nzuri ya kujiamulia mengi kuhusu watusika wa kazi hiyo.

Mhusika hupewa nafasi ya kuzungumza katika ulimwengu wake wa hadithini na maneno yake yakamweleza na kumpambanua zaidi, kwani tunatumia kauli zake mbalimbali kumtathmini. Kwa mfano, tutamtizama mtu anayetumia maneno ya matusi tofauti na mhusika ambaye anatumia lugha nyenyekevu. Mwandishi anapaswa kuwaacha watusika wake waongee katika majibizano au mazungumzo, kisha sisi wasomaji tuyatufute mawazo yao pamoja na misimamo yao kuhusu maswala kadhaa maishani. Aidha, tutaelewa vizuri mielekeo yao pamwe na mahusiano waliyonayo na watusika wenzao: wana uhasama, urafiki wa kweli au wa kinafiki? Wanapendana ama wanachukiana? Tutategemea maoni, mawazo na kauli kadha wa kadha anazozitoa mhusika sambamba na maoni, mawazo na kauli za watusika wenzake kuunda picha mahsusii ya mhusika huyo akilini mwetu.

Njia hii hujitokeza kwa uzuri zaidi iwapo hadithi inasimuliwa na mhusika mwenyewe katika nafsi ya kwanza. Kwa mfano Kazimoto na Manase wa *Kichwa Maji*, na msimulizi katika hadithi za "Roho Nyeusi" na 'Nitakuja kwa Siri', katika *Nitakuja kwa Siri* (1981). Itokeapo hivyo, mhusika mwenyewe anajieleza kwa mapana na marefu na kutujuvya hulka yake.

Mhusika Kufafanuliwa na Watusika Wenzake

Ijapokuwa mara kwa mara maelezo kuwahusu watusika katika hadithi hutolewa zaidi na msanii mwenyewe, anaweza pia akatumia maelezo ya watusika kuwafafanua watusika wenzao (Perrine 1966; Scott na Madden 1960, Hawthorn 1985). Mbinu hii ni ile ambayo inampatia mhusika au watusika fursa ya kutujulisha mengi kuhusu watusika wenzao katika mazungumzo yao hadithini. Kimsingi haya maelezo ya watusika wengine huwa ya ziada tu. Kwa mfano, katika *Kiza katika Nuru* (1988) tunaifahamu tabia ya mzee Juba kwa msaada wa mazungumzo ya watu waliokuwa wameketi kwenye ubao wakisubiri kumuona ofisini, na kumjua hata kabla ya kukutana naye riwayani.

Uwasilishaji Katika Matendo

Watusika huweza pia wakawasilishwa katika matendo. Mbinu hii inapata nguvu kutokana na imani kuwa matendo huwaeleza binadamu vizuri zaidi kuliko anayoyasema au wanayoyasema wengine kumhusu. Hili si ajabu kwa sababu

kuna wengi sana ambao hutenda kinyume na wanavyosema. Katika mbinu hii, mwandishi huyabania maelezo yake na kutuacha kumfahamu mhusika wake kwa kufuutilia matendo yake yanayotolewa kidogo kidogo hadi mwisho wa hadithi. Wasomaji tunapaswa kuyachunguza matendo ya mhusika katika miktadha mbalimbali na kujiamulia namna ya kumwelewa mhusika huyo.

Kulingana na Carpenter na Neumeyer (1974), mtazamo wetu wa watu hutegemea zaidi matendo yao. Wasomaji tuna jukumu la kuchunguza matendo ya wahusika na kuona kama yanaoana au yanakinzana na maneno yao. Kisha tujitahidi kutambua ni kwa namna gani kuoana au kukinzana huko kunatusaidia kuwafahamu zaidi wahusika hao. Hapa, msanii hutuonyesha badala ya kutueleza wahusika wake. Labda hii ni njia bora kwa vile inawawezesha wasomaji kuwatathmini wahusika wa hadithi maalum kulingana na mazungumzo pamoja na matendo yao. Aidha, Lewis na Altenbernd (1963) wanasema kuwa mbinu hii ni bora kwa sababu huturuhusu kujijengea maoni yetu kuwahuwu wahusika badala ya kuelekezwa na mwandishi. Hata hivyo, uwezo wetu wa kujiamulia hutingwa kwa sababu wahusika ni viumbe wa mwandishi ambaye ana uhuru wa kuwachotea na kuwachorea yote anayotaka wayawasilishe kwa ulimwengu wa wasomaji. Hivyo msanii anaamua mhusika wake atakachowaza na kutenda.

Mbali na hayo, mwandishi anapowasilisha wahusika wake kwa maelezo yake, kuna uwezekano mkubwa wa kuwachosha wasomaji. Kwa maana hiyo, waandishi wengi huzichanganya mbinu zote za uwasilishaji wa wahusika.

Aina za Wahusika

Wahusika katika kazi za fasihi hutofautiana kutokana na uumbaji wao, uwezo wa msanii, na jukumu ambalo wamekabidhiwa kulitekeleza katika kazi hiyo. Kimsingi kuna wahusika wakuu na wahusika wasaidizi. Wahusika wakuu huitawala hadithi nzima kwani hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Wanakuwa wahimili wa kazi husika kwani maudhui yake huwazunguka wao. Katika hadithi fupi, aghalabu mhusika mkuu huwa mmoja japo si ajabu kupata wawili au zaidi. Wahusika wadogo hujitokeza mara chache hadithini wakiwa na jukumu muhimu la kusaidia uelewekaji wa hadithi kwa kujenga dhimira ya kazi hiyo. Kando na huo mgawanyo wa kijumla, kuna aina zifuatazo za wahusika.

Wahusika Mviringo

Wahusika mviringo huitwa pia wahusika duara. Hawa ni wahusika ambao huyabania kulingana na matukio yanayowakuta katika ulimwengu wao wa hadithi. Wahusika hawa huaminika zaidi kwa sababu wanaonyesha tabia mbalimbali kama iliyovo katika maisha ya kawaida. Mhusika mviringo huzaliwa,

akakua, na anazokumba lazima mwake. Aidha binadamu hamaishani, hahizo katika wa Rosa Mi

Wahusika l
Wahusika b
au wazo m
hawabadilik
mabadiliko
1985, Msok
simulizi. Kv
Sungura aki
wahusika a
wachawi. W
zimetajwa k
kutoka mwa
Mifano ni v
Mohamed S
hawaelekei
ameligawa k
vielelezo. W
kuna aina
kuwaainisha.

Wahusika k
Hadithi fupi
mrefu sana
ngano, hadith
kuja kuibuka
sasa, yapo
maeneo amb
Uumbaji na
sana. Wahus
miungu na ha
wa kawaida l

akakua, na wakati mwingine akafa; almuradi hubadilika kutokana na hali tofauti anazokumbana nazo. Hata hivyo, mabadiliko haya hayapaswi kutokea tu. Ni lazima mwandishi atuonyeshe kichocheo cha mabadiliko hayo katika mhusika wake. Aidha, mabadiliko hayo ni muhimu yakuzwe hatua kwa hatua, kwani binadamu habadiliki kufumba na kufumbua. Kwa vile wahusika ni kama watu maishani, haiwezekani wakawa wabaya tu au wazuri tu bali watachanganya sifa hizo katika hayo mabadiliko yao. Mifano ya wahusika mviringo ni kama Rosa wa *Rosa Mistika* na Rehema katika *Nyota ya Rehema*.

Wahusika Bapa

Wahusika bapa huumbwa na msanii kwa madhumuni ya kuwakilisha dhana, sifa au wazo moja katika hadithi nzima. Tabia yao inabakia kuwa ileile na wala hawabadiiliki licha ya mahusiano yao na wahusika wengine au kutokana na mabadiliko katika mazingira yao (Lyon na Leslie 1963, Senkoro 1982, Mlacha 1985, Msokile 1992). Mbinu hii ya uumbaji wa wahusika imetokana na fasihi simulizi. Kwa mfano katika ngano, wahusika waliwakilisha tabia moja maalum. Sungura akiwakilisha ujanja ilhali fisi akawakilisha ulafi. Aidha, kulikuwa na wahusika ambao walikuwa wazuri tu na wale waliokuwa waovu tu kama wachawi. Wahusika bapa hawakui wala kupevuka. Riwaya nyingi za Shaaban zimetajwa kama mifano ya hadithi zenyé wahusika bapa; baadhi ni wazuri kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi na wengine ni wabaya kote hadithini. Mifano ni wahusika Majivuno, Utubora, Adili, Karama na kadhalika. Naye Mohamed Said Abdalla ana wahusika kama Msa na Spekta Seif ambao hawaelekei kubadiliki sana katika nyingi ya kazi zake. Mlacha (1985) ameligawa kundi hili mara mbili. Anasema kuna wahusika bapa sugu na bapa vielelezo. Wapo pia wahusika wafoili wanaojitokeza katika fasihi. Kwa hakika kuna aina nyingi ya wahusika kwa kutegemea vigezo vinavyotumiwa kuwaainisha.

Wahusika katika Hadithi Fupi

Hadithi fupi kama tuijuavyo hivi sasa ina asili yake katika utamaduni wa muda mrefu sana wa kusimuliana hadithi katika jamii mbalimbali. Awali zikiitwa ngano, hadithi za mapokezi zimepitia vipindi mbalimbali vya maendeleo hadi kuja kuibuka hadithi za kubuni. Katika maendeleo yake kufikia hali yake hivi sasa, yapo mabadiliko kadhaa yaliyoikumba hadithi fupi. Mionganoni mwa maeneo ambayo yamepitia hayo mabadiliko ni kipengele cha wahusika. Uumbaji na uwasilishaji wa wahusika wa hadithi fupi umekua na kubadiliki sana. Wahusika wa ngano waliweza kuwa; wanyama, miti, mimea, wadudu, miungu na hata majini. Wahusika hawa walipewa uwezo wa kiungu, usiokuwa wa kawaida hata kidogo. Hatimaye ngano zilianza kutumia mchanganyiko wa

wahusika wanyama na binadamu kueleza hali ya maisha ya binadamu. Mfano wa hadithi ya aina hiyo ni "Mvuvi na Jini", katika *Hekaya za Abunuwas na Hadithi Nyingine*. Ina mvuvi, ng'ombe, mnazi pamoja na watu watatu. Aghalabu, wahusika katika hadithi za mapokeo walikuwa hawapewi majina maalum. Majina yalikuwa ya kijumla kama vile; mfalme na malkia, mkulima na mkewe, mvuvi mmoja na kadhalika. Japo matumizi ya wahusika wanyama hayapatikani katika hadithi za kisasa, hutokea wakatumika mara mojamoja. Kwa Mfano, katika gazeti la *Kiongozi*, toleo la Novemba 16-30, 1993, Msokile ana hadithi iitwayo "Fisi ataka kumwondo Simba madarakani". Ingawa wahusika ni wanyama yanayojadiliwa yanalenga jamii ya wakati huo moja kwa moja. Hadithi nyingi za kubuni hivi sasa zinatumia wahusika watu katika hali ya kumulika maisha kihalisia.

Japo wahusika katika hadithi fupi pamoja na kazi nyingine za fasihi hawajitokezi wazi wazi kwa hadhira kama wanavyofanya wahusika wa tamthilia, hasa inapoigizwa jukwaani, wana nafasi muhimu sana katika kuisuka hadithi fupi na kuongoza mtiririko wa matukio yake. Tunapata ujumbe wa hadithi fupi kutokana na sifa, mazungumzo pamoja na matendo ya wahusika.

Wahusika ni kipengele kimojawapo muhimu sana ambacho huibainisha hadithi fupi na kuitofautisha na maandishi mengine ya nathari. Hadithi huumba wahusika kwa namna tofauti katika vipengele mbalimbali vyta uumbaji wa wahusika. Wataalamu wengi wa hadithi fupi wamesema kwamba, kwa kawaida, wahusika wa hadithi fupi hawakuzwi na kuendelezwa kikamilifu kama inavyokuwa katika riwaya au tamthilia. Sababu kubwa inayozua hali hii ni mawanda mafupi ya hadithi fupi. Mawanda hayo humnyima msanii fursa nzuri ya kuwachora wahusika wake kwa mapana na mafupi (Perrine 1960; Senkoro 1982; Msokile 1992).

Wahusika katika Hadithi Mahsusi

Katika hadithi ya "Siri ya Bwanyenye" ya M. Mulokozi, mhusika mkuu ni Niyetu. Katika kumuumba, kwa kiwango kikubwa, mwandishi amemfafanua Niyetu kutokana na maelezo yake (mwandishi). Tunafahamishwa wazi wazi kuwa hapo awali, Niyetu alikuwa mtu wa kawaida, tofauti na wakati huu anapongoza maandamano huku amevaa suti ya kitaifa na kushikilia bakora ya kipusa. Mara moja tunafahamikiwa kuwa ana hali nzuri maishani na ni kiongozi. Mengine anayotufahamisha mwandishi kumhusu Niyetu ni pamoja na: uwezo wake wa kutoa hotuba na kuwateka wasikilizaji; nyadhifa mbalimbali shikilia hadi sasa kuwa mbunge; ndoto zake za kupata uwaziri baadaye; uniko lake pamoja na gari lake aina ya benz; mandhari ya nyumba yake, pamoja na wiliwimmo ndani ya nyumba hiyo. Maelezo hayo ya kina ya mwandishi kumwelewa vizuri mhusika huyu.

Vilevile, Bi. Kessy, mkewe Niyetu ametolewa maelezo muhimu na msanii. Ni mkewe wa pili, mwenye elimu aliyeolewa baada ya mke wa kwanza kutilikiwa. Ni mwanamke kijana mwenye uso mzuri uliowazuzua na kuwababaisha wanaume. Tunaelezwa kuhusu madai kuwa alitoa mimba na kuharibu uzazi akiwa chuoni; hali ambayo inabainisha ni kwa nini hawajapata mtoto japo wameoana kwa miaka saba. Tunafahamishwa kuwa alikuwa ameavaa viatu vya mchuchumuo vilivyomfanya atembee kwa taratibu huku amebeba mkoba wa ngozi uliorembwa kwa madini ya kung'ara. Maelezo tunayotolewa kuhusu mhusika Salama ni machache sana. Alikuwa mtoto wa mke wa kwanza wa Niyetu na, atajwapo mara ya kwanza tunaambiwa kuwa anasoma shule ya sekondari. Mwandishi anatufunulia pia kuwa msichana huyu alikuwa na muamko na mchemko wa kisiasa na aliwahi kushikilia nyadhifa mbalimbali katika umoja wa vijana shulenii na hatimaye katika ngazi za wilaya.

Hatugusiji hata kidogo sifa zozote za umbo lake na, hadi mwisho wa hadithi, hatuelewi kama Salama ni mweusi au mwekundu, mrefu au mfupi na kadhalika. Kutokana na maelezo ya waandishi wasomaji huweza kuwaona wahusika wa kazi mbalimbali za fasihii na hata kuwalinganisha na watu mahsusii tunaoishi nao humu dunianai. Kutokana na maelezo finyu ya Mulokozi, tumenyimwa nafasi ya kumtambua Salama katika misingi hiyo. Aidha, hakuna popote hadithini ambapo tunakutana na Salama akizungumza na wahusika wengine ana kwa ana. Mara ya kwanza anaposhiriki katika mazungumzo ni pale wanapoongea na babake kwenye simu. Kwa hakika hiyo ndiyo inakuwa mara ya mwisho pia kwa sababu mazungumzo yake na Bi. Kessy tunaelezwa tu na mwandishi.

Imebidi tuwe na subira hadi mwishoni mwa hadithi ambapo mwandishi anampa Salama nafasi ya kujieleza zaidi kupitia yale aliyoyatenda. Matendo hayo anatufahamisha mwenyewe wakati anapozungumza na Niyetu kwa simu. Tendo lake la kuzigawa ovyo pesa za babake, huku akisema alidhani hawazihitaji kidogo limekithiri hali halisi ya Tanzania ya wakati huo. Hata hivyo, matendo yake yanatudhihirishia kuwepo kwa kizazi cha vijana waliojikomboa na ambaa ni wazalendo wanaojali maslahi ya umma zaidi ya maslahi ya kibinagsi.

Jina la mhusika huyu pia linasaidia kumweleza kwa wasomaji. Anaitwa Salama, lakini salama hii ina ncha mbili. Kwa upande wa Niyetu hakuwa salama hata kidogo kwani amezigawa ovyo pesa zake kwa "wanaharamu." Kwa upande wa umma Salama alikuwa mtunzaji salama wa mali ya umma.

Wapo wahusika wengine kadhaa waliosaidia kuikamilisha hadithi hii. Hawa wametajwa tu na mwandishi na wala hawakutolewa maelezo zaidi kwa namna yoyote. Hawa ni pamoja na katibu wa TANU wa wilaya, mwenyekiti wa TANU, pamoja na waheshimiwa wengine waliosubiri waandamanaji pale

juwaaani. Wengine ni wananchi walioshiriki katika maandamano, dereva wa Niyetu, na watumishi wake wa nyumbani.

Hadithi ya "Kicheko cha Ushindi" ya M.S. Mohamed ina wahusika wawili muhimu: Rajabu na Subira. Fatuma na Bi. Khadija ni wahusika wanaotumiwa ili kusaidia kuikamilisha hadithi hii na kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Kwa kiasi kikubwa, welewa wetu wa Rajabu umetokana na maeleo ya mwandishi. Hata hivyo, hatuelezi mengi sana kumhusu Rajabu kama mtu: yaani umbo lake, tabia yake, mazoea yake, na kadhalika bali anatufunulia anayokumbana nayo. Mohamed anaingia akilini mwa mhusika wake na kutueleza mawazo yake mbalimbali kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi.

Rajabu anahangaika sana kwani mkewe hajulikani alipo. Mwandishi ametueleza wasi wasi wake mwingi lakini muhimu zaidi ni kwamba kupitia kwa matendo yake tunapata kuielewa hali aliyokuwa nayo vizuri sana. Rajabu anaanza msako ambao unampeleka kwa Fatuma na Khadija. Anapomkosa mkewe katika hizo sehemu mbili anaweweseka mno. Anarejea kwake na mwishoni mwa hadithi tunamuona akilia. Maeleo ya mwandishi na zaidi matendo yake yanatudhihirishia thamana kubwa aliyokuwa nayo Subira kwa Rajabu. Imani yake ya dini inatajwa kwa mara ya kwanza na mwandishi lakini baada ya hapo msanii anatupa fursa ya kuiona imani hiyo katika maisha yake. Upo wakati ambapo Rajabu alikuwa mwingi sana wa mawazo kuihusu imani yake. Aidha, kuna wakati anaenda msikitini kwa sala ya isha ilhali hajui mkewe alipo. Hili bila shaka ni dhihirisho la imani kuu aliyokuwa nayo.

Katika hadithi nzima, Rajabu anazungumza mara chache sana. Mwanzoni akimtolea Subira masharti na wakati anapoenda kumsaka kwa Fatuma na Khadija. Akiwa nyumbani kwa Khadija anasema yafuatayo:

na...nam...sikuja kama...kama...Mungu akipenda...' Rajabu hakujua
aseme nini (uk. 5)

Hali nzima ya Rajabu kushindwa la kusema inatudhihirishia ile vuta nikuvute aliyokuwa nayo akilini. Alitarajia kumpata Subira hapo lakini hampati, anakuwa kama mtu aliyechanganyikiwa. Tunapata kuielewa hali yake zaidi kumokana na kauli ya Khadija anayemsikitikia kwa kupigwa na baridi ya kipupwe. Ni kweli kuwa Rajabu hajapewa fursa ya kujiyeza mwenyewe sana lakini msanii amefaulu kutufahamisha mengi kumhusu kwani anaingia hata akilini na kutufunulia yale anayoyawaza Rajabu. Kwa hivyo, kufikia mwishoni zote hadithi tunemwelewa hasa kulingana na nafasi yake katika hadithi ya "Kicheko cha Ushindi".

Subira ndiye sababu ya matatizo yote ya Rajabu katika hadithi hii lakini mhusika haya ametajwa tajwa tu bila ufanuzi mpana. Tunamtegemea zaidi

msanii kumjua Subira. Tunaambiwa kuwa aliyajua mapenzi ya mumewe kwake na ndiyo maana akaazimia kumtia adabu badala ya kujirahisisha kwake. Mwandishi anaieleza azma yake hivi:

potelea mbali juu lichomoze na yeye akose mume! Ulimwengu wenyewe ungekuwa tayari kupiga goti na kuuramba unyayo wake, naye katu asingekuwatayari kujirahisisha kwa Rajabu (uk.2).

Tunaambiwa kuwa alikuwa na kedi na majivuno. Zaidi ya kuambiwa hayo na mwandishi, Subira hajasawiriwa na kuwasilishwa kwa hali inayoonyesha hayo majivuno yake. Hazungumzi wala kuzungumzwa ili tumuelewe kama mwenye maringo. Labda tuchukulie kuwa kule kujificha na kumcheza shere mume wake ni mojawapo ya matendo yake ya kimaringo: lakini, vinginevyo hayo maringo yake hayaonekani katika uhusika wake. Subira hajazungumza kamwe hadithini, na hili huenda ni kwa sababu alipaswa kuwa amejificha. Tunapata fununu ya tabia yake kutokana na mhusika mwingine. Khadija anasema yafuatayo:

...nilijua Subira atakuwa mwandani kama sisi wazee wake. Mtazame alivyo' yeye na kwake, na kwake 'na yeye. Kwa nini usiniletee; namtamani? (uk. 5).

Ni wazi kutokana na kauli hiyo kuwa Subira hakuwa mtu wa kutembea ovyo. Imetajwa pia kuwa Rajabu ameamua kusoma kasida Subira aanzapo ulimi wake. Hili latujuvya kwamba Subira alikuwa msema mengi ama mtu wa kugombanagombana na mumewe. Ni hayo tu tuyajuayo kumhusu mhusika huyu.

Kulingana na mawazo ya Rajabu, ambayo tunaelezwa na mwandishi, Fatuma aliishi katika mtaa wa fujo nyingi na nyumba yake ilikuwa na desturi ambazo zilikuwa kinyume na desturi za kawaida. Hili latufanya tumuone kama mwananmke aliyeshiriki katika aina fulani ya maovu. Si ajabu Rajabu alihofia sana uwezekano wa Subira kuwa kwa Fatuma ambaye alimuona kama nazi mbovu. Pamoja na hayo maelezo ya mhusika mwenzake, msanii amempa fursa ya kujifafanua kupitia kwa mazungumzo yake na Rajabu. Anapomkaribisha Rajabu anasema hivi:

Ah, shemeji umekuja tena? (Uk. 3).

Kwa kawaida wageni hawakaribishihi hivyo. Anamfahamisha kuwa Subira ameishaondoka kwa sauti ya kutojali huku akiendelea kukipuliza chetezo, kisha kwa bezo anamnong'onezea Rajabu kukaribia ndani. Hayo yanatufanya tujue ni mwanamke wa aina gani.

Bi. Khadija tunamjua awali kutokana na mawazo ya Rajabu. Kulingana na Rajabu ingekuwa bora zaidi iwapo Subira angekimbilia kwa Khadija badala ya Fatuma kwani alimuona kama mtu mwema. Mawazo ya Rajabu yanathibitishwa tukutanapo naye hadithini baadaye. Ni mwislamu mwenye kufuata imani ya dini hiyo. Rajabu anapoingia na kumkuta akisali, anaendelea na sala bila kumjali mgeni aliyeingia. Mara tu anapomaliza kusali anasema hivi:

Ah, mwanangu Rajabu, karibu (uk. 5).

Anasisitiza kuwa ni lazima amtengenezee mgeni wake chai. Kwa jumla mazungumzo yake na makaribisho anayompa Rajabu yanatuonyesha kuwa ni mama mtaratibu, na mwenye heshima nyingi sana. Bi. Khadija na Fatuma wametenda na kuzungumza zaidi ya Subira katika hadithi hii na kwa hivyo uhusika wao unakuwa hai zaidi.

Katika "Arusi", hadithi ya Mbatiah, wahusika wake wameumbwa na kudhihirishwa kwa wasomaji zaidi kwa maelezo ya mwandishi. Kazi wanazozifanya Kibwi, Kathuure, Miriti, na Kanana tumejulishwa na msanii. Tunajulishwa pia majukumu waliyokuwa nayo Miriti na Kanana katika arusi ya Kibwi na Kathuure, pamoja na ukweli kuwa hao wawili walikuwa hawajakutana kabla ya hapo. Kibwi ameellezwu kwa kikamilifu sana. Tunafahamishwa kuhusu umbo lake; mavazi, sura, namna meno yake yaliyyokuwa yanang'ara na kadhalika. Aidha, Bibi arusi Kathuure amefafanuliwa kwa kirefu, hasa kuhusu urembo wake na ukweli kuwa walimtaka wengi naye akawakataa wote isipokuwa Kibwi.

Kumhusu Miriti, yapo mengi pia ambayo tumefahamishwa na msanii. Mwandishi anatufunulia mawazo yake kuhusu mahusiano ya vijana yanayoanzia shereheni na kukomaa hadi kuzua ndoa nyingine. Aidha, tunajuvvywa wasi wasi wake mkubwa baada ya kupokezwa barua ya rafikiye. Maendeleo ya uhusiano wao na Kanana baada ya arusi ya Kibwi yanawekwa wazi na msanii wa hadithi hii. Miriti anasikitika sana wakati ambapo babake anamwambia kuwa ndoa yake na Kanana hataibariki. Maelezo yanatolewa kuhusu arusi, hatima yake ya ghafla na maafa yaliyoitibia arusi hiyo.

Naye mtunzi wa "Walicheka Kicheko", John Habwe, ameitumia mbinu hii pia kuwaumba wahusika wake. Mapenzi na maisha mazuri ya ndoa waliyoishi Mogambi na Zainabu yanaelezwu na mwandishi kwa kuititia msimulizi. Mogambi alikuwa hatoki sana na kila mara walikuwa na mkewe nyumbani. Ilikiwa kiasi cha babake kuwalalamikia hirimu zake Mogambi kuhusu suala hilo. Bauliye kidogo msimulizi anatufunulia hali iliyozua kucheleva kwa Mogambi kuhusu nyumbani. Tunapata kufahamu awali kuwa alikuwa ameazimia kuchelewa makusudi. Alikunywa moja tu na kujimwagia pombe, kisha akasubiri mmoja upite. Wakati mkewe akihangaiya nyumbani, kabla ya Mogambi kwenda

nyumbani na kujiri ya kujiri, tayari sisi tuna fununu kuhusu maamuzi yake. Aidha, maelezo yametolewa kuhusu mchuano uliotokea baina ya Zainabu na Mogambi anaporudi nyumbani.

Mbatiah hakutumia mbinu moja tu kuwajenga na kuwawasilisha wahusika wake. Anawapa Miriti na Kanana fursa nzuri sana ya kuzungumza (uk.14-16), na kutokana na haya mazungumzo yao tunapata kuwaelewa zaidi na kufahamikiwa kuhusu kujengeka kwa huba baina yao. Aidha, wakutanapo kama walivyokuwa wameahidiana (uk.17-19), wanajifafanua zaidi kwa majibizano yao. Tunajulishwa makazi ya Kanana, uamuzi wa Miriti kuwa angetaka kumuoa, pamoja na jibu la Kanana kwa Miriti. Mwandishi wa hadithi hii pia ametumia barua kama mbinu nzuri ya kuwaeleza wahusika wake. Kwa hakika yaliyo kwa barua tunayajua kuitia kwa mwandishi lakini huu ni uamuzi mzuri unaopunguza uwezekano wa msimulizi kutuchosha kwa maelezo yanayofululiza moja kwa moja. Kuitia kwa hiyo barua tunapata kufahamu kuwa: Miriti haamini mambo ya ushirikina wala dini; kuwa Kibwi na mkewe wanamuenzi sana Miriti kama rafiki; wanakumbuka aliyowafanya katika arusi yao na wako tayari kumfanyia vivyo hivyo wakati wake ukifika. Kwa hivyo, wanajidhihirisha kama watu wema wanaokumbuka wanayotendewa na wenzao. Barua hiyo hiyo inatufunulia kuwa Kibwi alikuwa muoga na hakutaka kumweleza rafiki yake mambo hayo wazi wazi. Aidha, ni kuitia baruani tunajulishwa mengi kuhusu historia ya familia ya Kanana ambao ni ‘ngirani’.

Majibizano baina ya wahusika mbalimbali yamejitokeza kwa kiasi katika hadithi ya “Arusi”. Miriti na babake wanazungumza kuhusu uamuzi wa Miriti kumuoa Kanana (uk.24-25), uamuzi ambao babake anaupinga vikali sana. Nao Miriti na Kanana wanazungumza kuhusu uamuzi wao wa kuoana (uk.25). Vivyo hivyo katika hadithi ya Habwe, “Walicheka Kicheko”, kuna matumizi ya mbinu nyingine kando na maelezo ya mwandishi. Kuna majibizano mafupi baina ya Mucheke na Zainabu (uk.46). Majibizano haya yanaiweka wazi zaidi hali ya Zainabu. Alikuwa ameudhika sana na ndio maana anamjibu Mucheke kwa mkato. Sikia anavyojisemea mara tu Mucheke anapoondoka:

Hawa ndio walioanza kumtoa mume wangu. Shemeji, shemeji. Huu ushemeji gani. Mimi sitaki kujabughudhiwa usiku na watu. Kwani hawajui alikowakamtafute huko? Na tena usiku huu, maskini wanamtafutia nini?(uk.46)

Mambo yanapokuwa magumu mwishowe, na Zainabu kuwa kwa atalemewa na kipigo cha Mogambi anadhihirisha ujanja wa hali ya juu kwenye kwa matendo yake. Zainabu anasingizia kuwa yeye ndiye anapigwa na kwani na kutoka nje huku akilia na kuwaita majirani wamsaidie.

Maaoni ya Jumla Kuhusu Wahusika wa Hadithi Fupi

Ni dhahiri kuwa waandishi wa hadithi fupi hawachoti kutoka kwenye ghala tofauti na wasanii wa kazi nyingine za fasihi wanapowaumba na kuwasawiri wahusika wao. Mbinu wanazozitumia ni zile zile zitumiwazo na wenzao katika tanzu nyingine. Wahusika wameumbwa kwa kutumia lugha na fikra wanazopewa na waandishi; maelezo mbalimbali ya wasifu wao; matendo yao tofauti tofauti; uteuzi mzuri wa majina n.k. Kwa mfano, matendo ya Salama yanaiweka wazi tabia yake ya kujitolea kutetea umma wa wanyonge; Fatuma anadhihirisha mienendo yake kupitia kwa matendo yake, naye Zainabu anatuonyesha ujanaja wake kwa kutumia mbinu hiyo hiyo.

Katika hadithi ya "Siri ya Bwanyenye", majina ya wahusika yanasaidia kuwaumba. Niyetu ni mbunge na anapaswa kuwajali wote lakini katika matendo yake ni kinyume cha hivyo kwani anayajali maslahi yake tu. Kwa maana hiyo, anajidhihirisha kama Niyangu badala ya Niyetu. Na usalama wa Salama unajitokeza katika ncha mbili. Kwa Niyetu salama si salama hata kidogo lakini kwa umma Salama ni mtunzaji salama wa mali ya umma. Subira wa "Kicheko cha Ushindi" amedhihirisha subira yake kwa kubaki mafichoni hadi mwishoni mwa hadithi. Mbinu kuu za kuwasilisha wahusika zimejitokeza pia katika hadithi fupi. Kuna uwasilishaji dhahiri kuitia kwa maelezo ya waandishi; wahusika wamejifafanua wenyewe kuitia kwa matendo na mazungumzo yao. Aidha, wahusika wamewaeleza wenzao katika mazungumzo yao hadithini. Ni kweli kuwa waandishi wengi wametumia maelezo kuwafafanua wahusika wao lakini, kama tulivyoona, wameichanganya na nyingine kama: majibzano ya wahusika; wahusika kuwaeleza wenzao; simu na barua kuwaeleza wahusika n.k.

Licha ya ukweli kwamba mbinu zitumiwazo ni zilezile, matumizi yake katika hadithi fupi yanadhihirisha upkee wa namna fulani. Kwanza kabisa, waandishi wengi hutumia zaidi mbinu ya kuwaeleza wahusika wao. Tunaelezwa si tu umbo la wahusika bali pia tabia zao, kazi wazifanyazo, mahusiano yao na wenzao, pamoja na mawazo yanayowapitikia akilini mwao. Pili, hadithi fupi zina wahusika wachache sana. Wahusika walio na nafasi ya msingi katika "Siri ya Bwanyenye" ni watatu: Niyetu, Bi. Kessy, na Salama. Wengine kama dereva na wetumishi wa nyumbani pamoja na mwenyekiti wa TANU wametajwa tu. "Kicheko cha Ushindi" ina wanne lakini wanaodhihirika wazi hadithini ni wetatu: Fatuma, Khadija na Rajabu huku Subira akieleewa tu na mwandishi na wahusika wenzake. Katika hadithi ya "Arusi", wahusika wanaofafanuliwa japo kiasi ni wame: Kibwi, Miriti, Kanana na Kathuure, ilhali hadithi ya "Walicheka Kicheko", ina jumla ya watatu tu: Zainabu, Mogambi na Mucheke.

Swalli la msingi la kuijiuliza ni kama tofauti katika usawiri wa wahusika wa hadithi fupi unaimilia hadithi fupi kwa namna yote kuwa kazi nzuri ya fasihi.. Licha itakwa mwafaka kwanza kuelewa ni kwa nini hali iwe ilivyo kwa

hadithi fupi. Miongoni mwa sifa kuu zinazoufanua utanzu wa hadithi fupi na kuutofautisha na nyingine ni pamoja na: mawanda mafupi, iktisadi ya maneno, ploti sahili na mtiririko wa moja kwa moja wa matukio, na ufupi kwa jumla. Tukizingatia hayo yote ni wazi kwamba tutatarajia usawiri wake wa wahusika uwe tofauti. Kwa mfano, ili kutimiza hitaji la mawanda mafupi na matumizi ya maneno machache ni lazima mwandishi wa hadithi abane maelezo yake katika ukuzaji na uwasilishaji wa wahusika. Lohafer, (Lohafer na Clarey, 1989:66) anatoa maoni yafuatayo:

Ufupi wa hadithi hauruhusu uwasilishaji mkamilifu wa wahusika kwa kueleza vipengele vyote muhimu. Hilo limetokana na historia ya hadithi ambayo kimsingi ilimsawiri mhusika akikimbana na tatizo fulani kwa wakati maalum badala ya kuendelezwa taratibu kiwakati.

Kwa hivyo, kando na uchache wao, wahusika wa hadithi fupi hawakuzwi kikamilifu. Mwandishi hana nafasi ya kuwakuza hatua kwa hatua. Hawapewi nafasi ya kukua na kujipambanua barabara. Mwandishi huwasilisha mienendo na tabia za mhusika katika wakati maalum kuhusiana na mgogoro mkuu wa hadithi husika.

Hitimisho

Wahusika ni kipengele muhimu sana katika ujenzi wa kazi yoyote ya fasihi. Makala hii imeonyesha hilo kwa kueleza majukumu yao mbalimbali katika kuifanikisha kazi ya fasihi. Mahsus, makala hii imeonyesha kwamba hadithi fupi, kama zilivyo kazi nyingine za fasihi huwa na aina mbalimbali za wahusika. Hadithi vilevile hutumia mbinu sawa na zitumiwazo na tanzu nyingine za fasihi kuwaumba na kuwasilisha wahusika wake.

Pamoja na ukweli kwamba, kimsingi, waandishi wa hadithi fupi huchota pale pale wanapochota waandishi wengine, kuna tofauti kadhaa zinazoibuka katika usawiri wa wahusika wa hadithi fupi. Kutokana na sifa zake kuu: ufupi, iktisadi ya maneno, na mawanda yake, wahusika wake huyazingatia maswala muhimu katika maisha yao ya hadithini kwa mkato. Hili linasababisha waandishi kuwaeleza zaidi wahusika wao lakini maelezo hayo sharti yatolewe kwa muhtasari. Licha ya hayo, wanazikoleza kazi zao ukwasi wa kisanii kwa kuchanganya mbinu hiyo na nyingine kama vile; wahusika kupewa nafasi kujifafanua kimazungumzo na kimatendo. Ni bayana vilevile kuwa hadithi fupi aghalabu huwa na wahusika wachache sana. Palipo na wengi, ni wachache tu wanaopewa nafasi muhimu katika kazi hizo. Kwa jumla, kuna tofauti katika usawiri wa wahusika wa hadithi fupi; hali inayochangia upkee wake.

Marejeo

- Altenbernd, L. na Lewis, L.L. (wh.), (1963), *Introduction to Literature: Stories.* New York: Macmillan Company.
- Carpenter, J. and P. Neumeyer (1974), *Elements of Fiction: Introduction to the Short Story.* Dubugue, Iowa: W.M.C Brown Company Publishers.
- Habwe, J. (2000), "Walicheka Kicheko", katika: *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation, uk. 45-49
- Hawthorn, J. (1985), *Studying the Novel: An Introduction.* New Delhi: Universal Book stall
- Hussein, E. (1969), *Kinjeketile.* Nairobi: Oxford University Press
- Kezilahabi, E. (1971), *Rosa Mistika.* Nairobi: Kenya Literature Bureau
- Kezilahabi, E. (1979), *Gamba la Nyoka.* Dar es Salaam: Eastern Africa Publications
- Kezilahabi, E. (1974), *Kichwa Maji.* Dar es Salaam: East African Publishing House
- Kitsao, J. (1980) *Tazama Mbele.* Nairobi: Heinemann Educational Books
- Lohafer, S. and E. Clarey (wh.) (1989), *Short Story Theory at a Crossroads.* London: Louisian State Univversity Press.
- Mbatia, M. (2000), "Arusi", katika: *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation, uk. 11-27.
- Mkangi, K.G.C. (1984), *Mafuta.* Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mlacha, S.A.K. (1985), "Wahusika Katika Riwaya za Kiswahili Tanzania (1970-1982)" katika: *Mulika 17.* Dar es Salaam: TUKI
- Mohamed, S. A. (1988), *Kiza Katika Nuru.* Nairobi: Oxford University Press.
- Mohamed, S.M. (1978), "Kicheko cha Ushindi." katika: *Kicheko cha Ushindi.* Nairobi: Shungwaya Publishers, pp. 1-6
- Mohamed, S.M. (1976), *Nyota ya Rehema.* Nairobi: Oxford University Press.
- Mohochi, E. S. (1995), *Fani katika Hadithi Fupi za Kiswahili.* Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Egerton.
- Msokile, M. (1981), *Nitakuja kwa Siri...* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Msokile, M. (1992), *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: D.U.P.
- Mulokozi, M.M. (1992) "Siri ya Bwanyenye." katika: *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: D.U.P., pp. 121-131.
- Ngugi, W. na Mugo, M.G. (1976), *Mzalendo Kimathi.* Nairobi: Heinemann Kenya.
- Perrine, L. (1966), *Story and Structure.* Harcourt, Brace & World, Inc.
- Scott, V. na Madden, D. (1960) *Studies in the Short Story.* New York: Holt, Rinehart and Winston.
- Senkoro, F.E.M.K. (1982), *Fasihi.* Dar es Salam: Press and Publicity Centre.